

# MABANDA NMB NEW ERA STATIONERY



BRELA REG: 472535, TIN: 141 735 136, BIGWA KISIWANI ~ MOROGORO MUNICIPAL

Email: [newerastationery@gmail.com](mailto:newerastationery@gmail.com), Mobile: 0769 384 883

DATE: 18<sup>th</sup> January 2024

## TANGAZO LA KAZI (WAFANYAKAZI WA STATIONERY) - 03

**Mabanda Nmb - New Era Stationery** ni taasisi iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria ya usajili ya majina ya biashara (**The Business Names (Registration) Act (Cap 213)** chini ya BRELA –**The Business Registration Licensing Agents** na kupewa namba za usajili Na: **472735** Taasisi hii inajihusisha na uchapishaji na uandaaji wa nakala mbalimbali. Hivyo basi uongozi unawakaribisha wataanzania wote wenye sifa kuomba nafasi za kazi, kama zilivyoainishwa katika tangazo;

## KATIBU MAHSUSI DARAJA LA III (WAFANYAKAZI WA STATIONERY) - NAFASI 05

### Sifa za kuingilia moja kwa moja:-

- i. Kuajiriwa wahitimu wa Kidato cha Nne (Form IV) waliohudhuria Mafunzo ya Uhazili na kufaulu mtihani wa Hatua ya Tatu. Wawe wamefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kiingereza maneno 80 kwa dakika moja na wawe wamepata mafunzo ya Kompyuta kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti katika program za **Windows, Microsoft office, Internet, E-mail na Publisher.**
- ii. **Waombaji walio na uzoefu wa kufanya kazi kwa muda mrefu kwenye stationery mbalimbali watapewa kipaumbele.**
- iii. Umri ni kuanzia miaka 18- 27 kwa jinsia zote kike au kiume.
- iv. Awe tayari kuhudumia wateja kidigitali ili kuendana na maendeleo ya sayansi na teknolojia (Kama mwombaji hataweza kuhudumia kidigitali asiombe kazi hii)
- v. Awe mwepesi wa kutumia kompyuta mpakato kwa haraka zaidi.
- vi. Awe tayari kufanya kazi kuanzia Saa 07:00 Asubuhi hadi 20:00 Jioni kwa siku sita za wiki (Jumatatu – Jumamosi) na Jumapili kuanzia saa 10:00 hadi saa 20:00 Jioni.

**NB: Mwombaji kama hataweza kuzingatia au kufika kwa muda elekezi, ASIOMBE KAZI**

### b) Kazi/Majukumu ya kufanya:

- i. Kuchapa taarifa na nyaraka mbalimbali za ofisi na za wateja.
- ii. Kuhudumia wateja katika mahitaji mabalimbali (Photocopy, printing, scanning, passport size, Maombi yote kwa njia ya mtandao)
- iii. Kusaidia kupokea wageni na kuwasaidia shida zao pamoja na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
- iv. Kusaidia kutunza taarifa/ kumbukumbu za ofisi na wateja.
- v. Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo ofisini.
- vi. Kusaidia kufikisha maelekezo ya Mkuu wake wa kazi kwa wasaidizi wake na pia kumuarifu kuhusu taarifa zozote anazokuwa amepewa na wasaidizi hao.

- vii. Kusaidia kusambaza nyaraka katika taasisi elekezi - mbalimbali
- viii. Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na Msimamizi wake wa kazi.

#### **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KWA WAOMBAJI:-**

- i. Waombaji kazi wote waombe kwa kufuata masharti ya **TANGAZO LA KAZI**,
- ii. Waombaji kazi wote wawe ni raia wa Tanzania tu.
- iii. Waombaji wote lazima waambatanishe wasifu binafsi (CV) wenye mawasiliano ya uhakika, **anuani, barua pepe na namba za simu**
- iv. Waombaji lazima waambatanishe nakala za vyeti vifuatavyo;
  - a) **Cheti cha Mafunzo ya Uhazili / Mafunzo ya komyuta.**
  - b) **Cheti cha mtihani wa kidato cha nne au sita.**
  - c) **Cheti cha kuzaliwa.**
- v. Hati ya matokeo ya kidato cha nne au sita (Result slip) haitafanyiwa kazi,
- vi. Kuwasilisha vyeti vya kughushi na maelezo mengine itasababisha kuchukuliwa hatua za Kisheria.
- vii. Waombaji ambao ni Watumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba nafasi hizi.
- viii. Waombaji wasio na sifa ikiwemo na umri hawaruhusiwi kuomba kazi na mwombaji akiruma maombi hayatafanyiwa kazi.
- ix. Waombaji waonyeshe wadhamini wawili na mawasiliano yao, **anuani na namba za simu.**
- x. Waombaji kazi wenye vyeti vya kidato cha nne na cheti cha Taaluma ambavyo vimepatikana nje ya nchi wahakikishe vimehakikiwa na Baraza la Mitihani la Taifa (**NECTA**) na Baraza la Elimu ya Ufundi la Taifa (**NACTE**).
- xi. Barua ya maombi iandikwe kwa **Kiswahili** au **Kiingereza** kwenda **Meneja mwajiri, Mabanda NMB New Era Stationery, Bigwa Kisiwani & Misongeni, Morogoro**
- xii. Watakaochaguliwa kufanya usaili watajulishwa tarehe ya usaili (Usaili kwa walio mbali utafanyika kwa njia ya mtandao)
- xiii. Waombaji kazi ambao maombi yao **hayatakidhi** vigezo vya tangazo hili **hayatafanyiwa** kazi.

***Mwisho wa kupokea maombi ya kazi ni tarehe 25 Januari 2024 Saa 15:37 Alasiri (Zingatia muda)***

- ❖ **Maombi yote yatumwe kwa Email: [mabandanmbjob@gmail.com](mailto:mabandanmbjob@gmail.com) au yaletwe ofisini Bigwa kisiwani (Miti mitatu) au Misongeni, Morogoro Mjini (**Mabanda NMB New Era stationery**)**
- ❖ **Waombaji wote watafanya usaili kwa vitendo (Practical)**
- ❖ **Waombaji wote walioko mikoani au mbali na ofisi zetu watafanyiwa usaili kwa njia ya mtandao.**

Exp. Joseph YM Mabanda

